# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 044 AGOSTI 2024

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY




## 1 WADAU WAHIMIZWA KUTOA MAONI YAO NA KUTEKELEZA MAAZIMIO YA MKUTANO IPASAVYO

## 2 TANZANIA YAWANOA WATAALAMU WA HALI YA HEWA AFRIKA KUHUSU MATUMIZI YA RADA ZA HALI YA HEWA



## 3 FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2024



KITAIFA

# WADAU WAHIMIZWA KUTOA MAONI YAO NA KUTEKELEZA MAAZIMIO YA MKUTANO IPASAVYO

**Dodoma**



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilikutana na wadau kutoka sekta mbalimbali nchini ili kujipanga na Utabiri wa Msimu wa VULI 2024 katika ukumbi wa PSSSF, jijini Dodoma, tarehe 19 Agosti, 2024.

Akifungua mkutano huo, Mwenyekiti wa Bodi ya TMA, Mhe Jaji Mshibe Ali Bakari, aliwahimiza wadau kutoka sekta mbalimbali walioshiriki katika mkutano huo kutoa maoni yao sambamba na kutekeleza maazimio ya mkutano yatakayoafikiwa.

"Tunapoelekea kutoa utabiri wa mvua za Vuli (Oktoba hadi Disemba), 2024 ninawahimiza wadau kutumia jukwaa hili katika kutoa michango ya maoni yenu kikamilifu ili kuleta tija kwa sekta mbalimbali nchini pamoja na kutekeleza maazimio yatakayofikiwa". Alisema Mhe. Jaji Mshibe.

Mhe. Jaji Mshibe alisisitiza kuwa matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa ni muhimu hususani katika kipindi hiki ambapo dunia pamoja na nchi yetu inakabiliwa na changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa.

"Ninapenda kutoa msisitizo kwenu, katika majadiliano ya mvua za Vuli ya mwaka huu, 2024, mjikite katika kujadili namna ya kuimarisha matumizi ya utabiri wa hali ya hewa

mtakaopewa na kushauri hatua stahiki za kuchukua". Alisisitiza Mhe. Jaji Mshibe.

Akizungumza awali Makamu mwenyekiti wa Bodi ya TMA, Dkt Emmanuel Mpeta, aliipongeza TMA kwa kazi nzuri ya kuimarisha ubora na usahihi wa utabiri hususan katika kipindi hiki ambacho Dunia inakabiliwa na mabadiliko ya hali hewa na kuwaomba wadau wa sekta mbalimbali kuwasilisha maoni yao ya kuimarisha ushauri kwa sekta na jamii.

Wakati akimkaribisha mgeni rasmi, Kaimu Mkurugenzi Mkuu, TMA na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Mabadiliko ya Sayansi ya Hali ya Hewa na Tabianchi, Dkt. Ladislaus Chang'a aliishukuru Serikali kwa kuendelea na uwekezaji katika miundombinu ya hali ya hewa hapa nchini, alisema kupitia jitihada hizo, Mamlaka imeendelea kuboresha na kuimarisha huduma za hali ya hewa ikiwemo kutoa taarifa za utabiri wa maeneo madogo madogo kwa wilaya zote 86 za mikoa iliyopo katika ukanda unaopata mvua za Vuli na hivyo kusaidia katika kufanya maamuzi stahiki kwa lengo la kuongeza tija na kupunguza madhara ya hali mbaya ya hewa inapojitokeza.

"Niishukuru serikali na wadau wa maendeleo kwa kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya hali ya hewa hapa nchini" Alisema Dkt. Chang'a.

Dkt. Chang'a aliendelea kusema kuwa mvua za Vuli ni mahsusi kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka ambayo ni Pwani ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki, na Ukanda wa Ziwa Victoria zenye mchango mkubwa katika sekta mbalimbali zikiwemo kilimo, nishati, maji n.k.

Aidha, ilielezwa kuwa taarifa sahihi za hali ya hewa pamoja na athari zake ni muhimu kupatikana kwa wote na kwa wakati ili kuwezesha jamii na wadau kujipanga na kuandaa shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo yao.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilitoa taarifa rasmi ya msimu wa mvua za Vuli tarehe 22 Agosti 2024.



## KIMATAIFA

# TANZANIA YAWANOA WATAALAMU WA HALI YA HEWA AFRIKA KUHUSU MATUMIZI YA RADA ZA HALI YA HEWA

**Mwanza**




Katika kuwajengea uwezo wataalamu wa hali ya hewa kutoka Taasisi za Hali ya Hewa barani Afrika, Kitengo cha Elimu na Mafunzo cha Shirika la Hali ya Hewa Duniani kwa kushirikiana na Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa kinachoendeshwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), waliandaa mafunzo mahsusi ya matumizi ya data na taarifa za Rada za Hali ya Hewa. Mafunzo hayo yalifanyika katika Ukumbi wa Malaika, Mwanza, tarehe 26 hadi 30 Agosti 2024.

Akifungua rasmi mafunzo hayo, Waziri wa Uchukuzi, Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb); alieleza lengo la mafunzo hayo ni kuimarisha zaidi uwezo wa wataalamu wa hali ya hewa na wataalam wengine husika kutoka baadhi ya Nchi za Afika Mashariki na Kusini mwa Afrika katika matumizi bora ya taarifa za Rada za hali ya hewa kwa ajili ya kuboresha utabiri wa hali ya hewa na utoaji wa tahadhari za matukio ya hali mbaya ya hewa kwa jamii.

Aidha, alieleza kuwa mafunzo hayo yaliendana na utekelezaji wa mpango ulioasisiwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa utoaji wa Tahadhari kwa Wote (Early Warning for All EW4ALL) ifikapo mwishoni mwa mwaka 2027, pamoja na Sera ya Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) ya ubadilishanaji wa data za hali ya hewa kimataifa ("WMO Unified Data Policy"). Mafunzo hayo yana umuhimu mkubwa kwa nchi wanachama wa WMO kanda ya Afrika (WMO RA1) katika kuongeza uwezo unaohitajika zaidi wa utoaji wa huduma za hali ya hewa na tahadhari kupitia taasisi za hali ya hewa za nchi

husika kukabiliana na ongezeko la idadi na ukubwa wa matukio ya hali mbaya ya hewa katika muktadha wa mabadiliko ya hali ya hewa na hivyo kuchangia kuokoa maisha ya watu na mali zao.

Alisisitiza umuhimu wa kufanya uwekezaji wa miundo mbinu ya kisasa ya hali ya hewa kama vile rada, alifafanua kuwa Tanzania imekuwa kielelezo bora katika kufanya uwekezaji huo pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wa hali ya hewa nchini, na hivyo kuchochea fursa ya kuandaa mafunzo hayo.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Mwakilishi wa kudumu wa WMO, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa naTabianchi, Dkt. Ladislaus Chang'a, alieleza kuwa TMA ilijiandaa vyema kupitia wataalamu wake katika kutoa mafunzo hayo "Wataalamu watakao toa mafunzo ni wabobezi, na kati yao wamepata mafunzo kutoka Marekani na Finland na vilevile ni wakufunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam". Alisema Dkt. Chang'a.



Kwa upande wake, Mwakilikishi kutoka WMO (Ofisi ya Mafunzo), Bi. Eunjin CHOI aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kufanikisha mafunzo hayo muhimu ya matumizi ya taarifa na data za rada za hali ya hewa. "Kupitia ushirikiano huu, kwa pamoja tunaweza kuendeleza malengo yetu ya kuboresha huduma za hali ya hewa, si tu kwa Tanzania bali duniani kote". Alisisitiza Bi. Eunjin.

Tanzania ilitoa mafunzo kwa wataalamu wa hali ya hewa kutoka baadhi ya nchi Wanachama wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) kanda ya Afrika ambao ni Burundi, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Msumbiji, Malawi, Mauritius, Rwanda, Seychelles, Sudan Kusini, Uganda, Tanzania na Zambia.



TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# FAHAMU ZAIDI

## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2024

Kipindi cha mwezi Septemba 2024, maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuendelea kuwa na hali ya ukavu na ongezeko kidogo la joto. Hata hivyo, hali ya baridi kiasi hadi baridi kali inatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi na Kusini mwa nchi hususan nyakati za usiku na asubuhi. Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo ya ukanda wa Pwani, Nyanda za Juu Kaskazini Mashariki na Ziwa Victoria. Kwa upande mwingine, vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| **Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18 °C hadi 26 °C katika maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani na kati ya nyuzi joto 14 °C na 24 °C katika maeneo ya nchi kavu. **Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi ikiambatana na vipindi vichache vya mvua katika maeneo ya mwambao wa pwani.** |
| **Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 22 °C katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 14 °C. **Kwa ujumla hali ya ukavu pamoja na vipindi vichache vya mvua hususan katika maeneo ya miinuko inatarajiwa kujitokeza.** |
| **Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 °C hadi 22 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 16 °C. **Kwa upande mwingine, vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika maeneo machache.** |
| **Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 22 °C katika maeneo mengi. **Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.** |
| **Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. **Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.** |
| **Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 8 °C hadi 16 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko (ikijumuisha mkoa wa Njombe) yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 8 °C. **Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.** |
| **Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 °C hadi 24 °C katika maeneo mengi. **Aidha, kiujumla hali ya ukavu inatarajiwa na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.** |
| **Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma):** | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. **Aidha, maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 12 °C. Hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi.** |

# UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO SEKTA YA HALI YA HEWA

## Vifaa vya utambuzi wa matukio ya radi

Mamlaka imefanikiwa kununua na kufunga seti tano (5) za vifaa vya utambuzi wa matukio ya radi (Lighting detectors) ambavyo vimefungwa katika maeneo ya Musoma, Mwanza, Kagera, Tabora na Kigoma. Mamlaka bado inahitaji seti 20 ili kukamilisha mtandao wa vifaa kwa ajili ya utambuzi wa Matukio ya radi.








**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Bakari Msambekwa
Monica Mutoni

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa

www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

TMAonline TV

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.